**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

**VETA IRINGA DVTC**

**BARUA YA KUJIUNGA NA CHUO NGAZI YA KWANZA IRINGA DVTC - 2026**

Ndugu, ......................................................................................................................................................

**YAH**: **KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI CHA WILAYA YA IRINGA (IDVTC) MWAKA 2026**

**MAELEZO HAYA YASOMWE KWA MAKINI NA MZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI**

1. Unafahamishwa kwamba umechaguliwa kujiunga na chuo tajwa hapo juu katika
2. Fani ya: ..........................................................................................................................

   Ngazi ya Kwanza **(Level One)** Kutwa/Bweni.........................................
3. Mafunzo yatachukua muda wa miaka miwili kwa ngazi mbili kwa fani ya
   i. USHONAJI NA UBUNIFU WAMAVAZI
   ii. UFUNDI UMEME
   iii. UFUNDI UASHI
   iv. UFUNDI MAGARI
   v. UFUNDI BOMBA
   vi. UCHOMELEAJI NA UUNGAJI VYUMA
4. Chuo kitafunguliwa rasmi Tarehe :**13/01/2026**
5. Unatakiwa kuthibitisha wewe **mwenyewe na mzazi/mlezi/mdhamini** wako kwamba unakubali nafasi ya mafunzo uliyopangiwa kwa kujaza fomu maalum iliyoambatanishwa kwenye barua hii.
6. Unatakiwa kufuata sheria na taratibu zote za chuo zilizoambatanishwa kwenye barua hii mara utakapofika chuoni.
7. Unatakiwa kufika chuoni na barua hii siku ya kuanza Mafunzo.
8. Unatakiwa kununua vifaa vilivyoambatanishwa na barua hii kwa matumizi yako chuoni.
9. Unatakiwa kuleta kivuli cha **cheti cha kuzaliwa** na **cheti kumaliza shule.**

**MAHITAJI YA MWANAFUNZI ATAKAPORIPOTI CHUONI**

***Unatakiwa uwe na vifaa vifuatavyo:***

1. Mashati mawili (2) meupe mikono mifupi ya "Tetron" **Kwa wavulana na wasichana.**
2. Jozi ya viatu vyeusi vya ngozi vya kamba na vyenye visigino vifupi kwa fani ya **ushonaji**
3. Jozi ya viatu vyeusi vya ngozi vya kamba vyenye visigino vifupi na jozi moja ya viatu vya kujikinga na hatari wakati wa mafunzo **(safety boot) kwa fani ya ufundi umeme,ufundi uashi (ujenzi),ufundi magari,ufundi kuchomelea na ufundi bomba**
4. Daftari 8 kubwa **(Counter Book)**
5. Vifaa vya Hesabu **(Mathematical set**)
6. Karatasi nyeupe **(A4) ream moja**
7. Sweta rangi ya Blue
8. Kwa mwanafunzi wa Fani ya **ufundi umeme** na **ufundi uashi (ujenzi)** aje na fagio (**Soft Broom**).
9. Kwa wanafunzi wa fani ya **ufundi bomba** na ufundi **magari** aje na **fyekeo (Kwanja)**
10. Kwa wanafunzi wa fani ya **ushonaji** na **ufundi wa kuchomelea** aje na fagio la kudekia (**Rubber squeezer**)
11. Kwa mwanafunzi wa bweni anataikiwa kufika na **mto wa kulalia**, **shuka rangi ya blue**, **chandarua**, **ndoo ya kufulia na kuogea**, **sahani, kikombe**, **kijiko**, nguo za kujikinga na baridi utakapokuwa bwenini, pamoja na **vifaa vya usafi binafsi**.
12. Mwanafunzi aje na nguo za michezo na viatu vya michezo.
13. Mwanafunzi aje na rain boots **(Mabuti kwaajili ya mvua)** pia kwa ajili ya shughuli za nje.
14. Mwanafunzi mwenye **bima ya afya (NHIF)** aje na kitambulisho cha bima ya afya.

***JEDWALI Na.01***

**MCHANGANUO WA MALIPO YATAKAYO LIPWA KWA CONTROL NAMBA**

| NA | MAHITAJI | KWA MWANAFUNZI WA BWENI | | KWA MWANAFUNZI WA KUTWA | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | MUHULA I | MUHULA II | MUHULA I | MUHULA II |
| 1. | ADA YA MAFUNZO | 60,000 | 60,000 | 30,000 | 30,000 |
| 2. | NEMBO ZA VETA | 5,000 | | 5,000 | |
| 3. | MICHEZO | 15,000 | | 15,000 | |
| 4. | FEDHA YA TAHADHARI | 20,000 | | 20,000 | |
| 5. | FULANA/T-SHIRT | 15,000 | | 15,000 | |
| 6. | KITAMBULISHO | 5000 | | 5,000 | |
| 7. | GODORO | 20,000 | | | |
| 8. | FEDHA ZA MAHAFALI | 10,000 | | 10,000 | |
| 9. | BIMA YA AFYA (NHIF) | 50,400 | | 50,400 | |
| | **JUMLA** | **200,400** | **60,000** | **150,400** | **30,000** |

i. Muhula wa kwanza Mwanafunzi wa bweni atatakiwa kulipia jumla **TSH 200,400/=**
   a. Ikiwa ada ya Mafunzo ni **TSH 60,000/=**
   b. Michango mingine **TSH 140,400/=**

ii. Muhula wa kwanza Mwanafunzi wa kutwa atatakiwa kulipia jumla TSH **150,400/=**
   a. Ikiwa ada ya Mafunzo ni **TSH 30,000/=**
   b. Michango mingine **TSH 120,400/=**

*JEDWALI Na.02*

**MCHANGANUO WA GHARAMA ZA UNIFOMU.**

<table>
<tr><td rowspan="2">NA</td><td rowspan="2" colspan="2">MAHITAJI</td><td colspan="2">KWA MWANAFUNZI WA KUTWA</td><td colspan="2">KWA MWANAFUNZI WA BWENI</td></tr>
<tr><td>MUHULA I</td><td>MUHULA II</td><td>MUHULA I</td><td>MUHULA II</td></tr>
<tr><td>1.</td><td colspan="2">Suruali **(2)** za chuo</td><td>50,000</td><td></td><td>50,000</td><td></td></tr>
<tr><td>2.</td><td colspan="2">Overcoat/Ovaroli</td><td>30,000</td><td></td><td>30,000</td><td></td></tr>
<tr><td rowspan="2"></td><td rowspan="2">***JUMLA***</td><td>***Wavulana***</td><td>***80,000***</td><td></td><td>***80,000***</td><td></td></tr>
<tr><td>***Wasichana***</td><td>***80,000***</td><td></td><td>***80,000***</td><td></td></tr>
</table>

## GHARAMA NYINGINE

I. Ada ya mtihani wa taifa wa VETA (CBA) ya **TSH. 25,000/=** kwa ngazi ya kwanza italipiwa muhula wa pili wa Mafunzo.

**MAELEZO MENGINE ZAIDI UTAELEKEZWA UFIKAPO CHUONI AU PIGA SIMU NAMBA 0620551878 au 0755292322**

Kwa niaba ya Chuo -Chuo Cha Wilaya Iringa DVTC

Petronila Shatta

Mkuu Wa Chuo

**IRINGA DVTC**

## VIAMBATANISHO

I. Medical Examinations form

II. Sheria za chuo

III. Fomu ya kukubali nafasi ya mafunzo ya ufundi

## CHUO CHA UFUNDI STADI IRINGA DVTC

## SHERIA ZA CHUO:

Iii kufanikisha mafunzo ya ufundi stadi kila mwanafunzi anatakiwa kufuata sheria zifuatazo:-

1. **MAHUDHURIO:**

   a. Kila mwanafunzi anatakiwa kufika chuoni kabla ya saa **1:30 asubuhi.** Hii ina maana ifikapo saa 1:30 asubuhi wanafunzi wote wawe wameshafika chuoni. Endapo mwanafunzi atachelewa adhabu kali itatolewa.
   b. Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya chuo kwenda nyumbani, hospitali Au sehemu nyingine yoyote ile bila ya kuruhusiwa na Mwalimu wa zamu kupitia kwa mwalimu wa darasa.
   c. Mwanafunzi apatapo matatizo ya msiba, kuuguliwa au kuugua mwenyewe ni lazima habari/taarifa zifike chuoni, bila ya kufanya hivyo ni kosa.
   d. Mahudhurio chini ya 85% mwanafunzi atanyimwa cheti cha kuhitimu mafunzo.

2. **MAVAZI:**

   a. Sare ya chuo ni suruali ya dark bluu na shati jeupe la mikono mifupi na T-shirt ya VETA. Sare hiyo ivaliwe wakati wote mwanafunzi awapo chuoni na wakati wa safari ya kuja chuoni na kurudi nyumbani. Wakati wote shati liwe limechomekewa.
   b. Ovaroli livaliwe wakati wa vipindi vya kazi za mikono tu.
   c. Viatu vyenye visigino virefu na kanda mbili au viatu vya wazi (sandals) haviruhusiwi kuvaliwa karakana.
   d. Vifaa vya usalama vivaliwe kikamilifu wakati wote wa mafunzo kwenye karakana.

3. **USAFI WA MWILI:**

   a. Hairuhusiwi kuvaa hereni, pete, bangili na mapambo ya aina yoyote ile kwa kipindi chote cha mafunzo. Hairuhusiwi kutumia vipodozi au manukato yanayotoa harufu kali.

   b. **NYWELE KWA WAVULANA:**
      i. Zikatwe ziwe fupi sana, KIPARA hairuhusiwi kabisa.
      ii. Ndevu haziruhusiwi. Ndevu za aina zote haziruhusiwi mustachi/sharubu
      iii.

c. **NYWELE KWA WASICHANA:**

iv. Zikatwe ziwe fupi au zisukwe kwa mistari ya kurudi nyuma zisizidi sita.
v. kucha zisifugwe kabisa wala kupaka rangi

4. **WIZI WA MALI ZA CHUO AU MALI YA MTU VEYOTE YULE:**

a. Vitendo vyote vya wizi haviruhusiwi. Pindi ikibainika mwanafunzi ameiba mali ya chuo au mwanafunzi mwenzake, basi atafukuzwa chuo mara moja na kufikishwa kwenye vyombo vya dola.
b. Ukipoteza kifaa cha chuo utatakiwa kulipa gharama kamili ya kifaa na ukakinunue kifaa chenyewe au ulete badala ya ulichokipoteza.
c. Hairuhusiwi mwanafunzi kuingia na kifaa chochote kile kinachofanana na vile vilivyoko ndani ya chuo.
d. Mwanafunzi atapekuliwa wakati wa kutoka karakana na getini.

5. **UGOMVI:**

a. `Ugomvi, kupigana au kushambuliana ni makosa ya jinai. Atakayepatikana akijihusisha na matendo ya namna hiyo atafukuzwa chuoni na kukabidhiwa kwenye vyombo vya dola

6. **ULEVI:**

a. Iwapo itabainika mwanafunzi analewa au kuonekana katika sehemu za vileo, anavuta bangi au madawa ya kulevya adhabu yake ni kufukuzwa chuo mara moja.

7. **MAPENZI:**

a. Uhusiano wa kimapenzi chuoni kati ya mwanafunzi na mwanafunzi au kati ya mfanyakazi/mwalimu na mwanafunzi hairuhusiwi kabisa.
b. Mwanafunzi wa kiume au wa kike haruhusiwi kuingia maeneo wanayoishi watumishi bila ya kibali au ruhusa.

8. **MIGOMO:**

a. Migomo ni marufuku, na kuchochea migomo ni kosa lisilostahimilika. Atakayeshawishi au kusababisha migomo atafukuzwa chuoni mara moja.

9. **LUGHA:**

a. Lugha inayotumika kwa mawasiliano iwe ya staha na sio ya matusi.

10. **KUBADILI JINA**

a. Jina lisibadilishwe mpaka ziwepo sababu na hati maalum kwa uthibitisho na ajulishwe Mkuu wa Chuo mara moja.

11. **MATUMIZI YA SIMU DARASANI**

a. Ni marufuku kuwasha simu za mkononi wakati wote wa vipindi.
b. Ni marufuku kuweka visikilizia sauti masikioni (Earpods na Earphones) wakati wote wa vipindi chuoni.

12. **USAFI WA MAZINGIRA**

a. Usafi wa maeneo yote ya chuo ni wajibu wa kila mwanafunzi hivyo unawajibika kila wakati kutunza bustani, kufagia na kufyeka nyasi maeneo yote ya ndani ya chuo na eneo linalozunguka chuo
b. Ni marufuku kushika au kukanyaga kuta za majengo maeneo ya karakana na ofisi
c. Huruhusiwi kukatisha maeneo ya bustani au sehemu zilizopandwa nyasi, unatakiwa kutumia njia husika tu.
d. Ni marufuku kuingia darasani au karakana na aina yeyote ya kimiminika, chakula, bazooka n.k
e. Unatakiwa kutupa takataka sehemu husika za kutupa taka na si vinginevyo.

**13**. Mwanachuo ataruhusiwa kutoka nje ya chuo kwa kibali maalum

**14**. **Mwanachuo** yeyote anayeruhusiwa kutoka nje ya eneo la Chuo anapaswa kuwa na kitambulisho cha Chuo na atajiandikisha lango kuu na sare ya Chuo. Mwanafunzi atakayeonekana nje ya maeneo ya Chuo bila kitambulisho atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa nafasi ya kulala bwenini au kufukuzwa chuoni

15. Hairuhusiwi kupikia chakula bwenini, na atakayekiuka sheria hii atachukuliwa hatua kali.

16(a) Ni marufuku wanachuo wa kiume na wakike kutembeleana mabwenini.

(b) Hairuhusiwi KABISA kwa mwanachuo kuingia katika eneo wanalo ishi wafanyakazi wa Chuo bila ruhusa au kibali.

**17** Hairuhusiwi kupeleka chakula bwenini. Endapo kuna mgonjwa, ruhusa maalum kutoka kwa Mwalimu wa zamu/Mlezi wa wanafunzi itatolewa.

**18** Taa za madarasani na mabwenini zizimwe **saa 4:00** za usiku.

**19.** Hakuna ruhusa kumkaribisha au kumlaza mgeni, ikiwa mwanachuo atatembelewa na mgeni au ndugu siku ya masomo, ni lazima kumjulisha mwalimu wa zamu kabla ya kumkaribisha katika sehemu ya mazungumzo.

**20**. Vyumba/Madarasa na vifaa vitumiwe kufuatana na shughuli zake. Hairuhusiwi kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya Chuo.

**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI-VETA**

**CHUO CHA VETA – IRINGA DVTC**

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

**A. MWANACHUO**

Mimi ............................................................................................... Ninakubaliana na nafasi ya mafunzo katika fani niliyopangiwa pamoja na kuzingatia sheria na kanuni za chuo ambazo nimezisoma na kuzielewa vizuri.

Namba za simu za mwanachuo: (i) ...................................... (ii)...................................

Saini ya mwanachuo .................................. Tarehe......................................

**B. MDHAMINI**

Mimi ................................................................................................................................ Ambaye ni ..........................................wa mtajwa hapo juu nimethibitisha kuwa nitamdhamini na kumlipia gharama zote za mafunzo, ikiwa ni ada na gharama nyingine kama ilivyoelezwa katika maelezo ya kujiunga na chuo na nauli ya kwenda chuoni na kurudi nyumbani wakati wote wa likizo na baada ya mafunzo.

Namba za simu ya mdhamini: (i)...................................... (ii)........................................

Saini ya mdhamini ...................................... Tarehe ...................................

## VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY

## MEDICAL EXAMINATION FORM

Date……………………………..

The Medical Officer

……………………………………………

……………………………………………

……………………………………………

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Name of trainee: …………………………………………………………….

Please Examine the above-named trainee to his/her fitness to undergo training and subsequently.
Work as/an………………………………………………………….

Eyesight…………………………………………………………….

Hearing…………………………………………………………….

Asthma…………………………………………………………….

Other serious diseases…………………………………………….

**MEDICAL CERTIFICATE:**

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for training as above.

Date: ……………………………. Designation ……………………………………….

Signature and Official Stamp…………………………………………….